**TAARIFA YA HALI YA UPATIKANAJI WA MAJI MANISPAA YA TABORA**






**July, 2017**

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa ya Tabora yenye km za mraba **1,090;** kwa sasa inakadiriwa kuwa na wakazi wapatao **261,267** kutokana na makisio ya idadi ya watu ya sensa ya mwaka 2012 ya watu 226,999 yenye ongezeko la watu **asilimia 2.9** kwa mwaka. Hata hivyo kunauwezekano idadi ya watu katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora itaongezeka kwa kasi kufuatia Taasisi mbalimbali kuonyesha dalili za kuwekeza Mjini Tabora, baada ya ujenzi wa barabara unaoendelea kukamilika. Mathalani, Chuo kikuu cha SAUT na TEKU tayari vimekwisha anzishwa na Taasisi nyingine kama vile; Chuo cha Ardhi, Chuo cha Utumishi wa Umma (UHAZILI), Chuo cha Nyuki na Chuo cha Ualimu Tabora zimekusudia kupanua huduma ambapo itapelekea kuwa na idadi kubwa ya watu na hivyo kufanya mahitaji ya Maji kuwa makubwa kuliko ilivyo hivi sasa.

Mahitaji ya Maji kwa Mji wa Tabora kwa sasa ni mita za ujazo **27,816** kwa siku, ambapo uwezo wa mitambo ya kuzalisha maji kwa sasa umeongezeka kutoka mita za ujazo **15,000** kwa siku mwaka 2015 na kufikia mita za ujazo **30,000** kwa siku, sawa na asilimia **107.9** . Pamoja na kuwa na mitambo ya kuzalisha yenye uwezo unaozidi mahitaji ya Manispaa kwa sasa, inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka **2020** mahitaji ya maji ya Manispaa (ambazo ni mita za ujazo **30,285** kwa siku) yatakuwa yamezidi uwezo wa uzalishaji wa mita za ujazo **30,000** kwa siku.

Hata hivyo kutokana na ufinyu wa miundombinu ya kusambaza maji katika maeneo mbalimbali ya Manispaa yakiwemo maeneo yanayoendelezwa kwa kasi, imepelekea kuwa na uzalishaji wa mita za ujazo takribani **16,500** kwa siku ili kukidhi mahitaji ya maji katika maeneo yaliyofikiwa na mtandao wa maji. Kwa hiyo huduma ya maji hutolewa katika kata **20** tu kati ya kata **29** zilizopo ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na ni asilimia ***84*** tu ya wakazi wa kata **20** ndio wanaopata huduma ya Majisafi na salama, na kata 9 zilizoko pembezoni mwa Manispaa, hupata maji kwa njia ya visima virefu na vifupi, ambavyo husimamiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

### 1.2 Vyanzo vya Maji

Vyanzo vikuu vya Maji katika Mji wa Tabora ni Maji yaliyo juu ya ardhi ambayo ni mabwawa ya **Kazima na Igombe,** yaliyoanza kutumika **miaka ya 1949 na 1958,** kwa mfuatano ambayo kwa kiasi kikubwa hutegemea hali ya mvua.

### 1.2.1Bwawa la Kazima

Bwawa la Kazima lililoko takribani **km 12** kutoka mjini Tabora barabara ya kuelekea Nzega, na lina uwezo wa kutunza mita za ujazo **1,620,000** kwa mwaka.

Licha ya Bwawa la Kazima kutumika kama chanzo, kina cha Bwawa kimepungua kutokana na kuongezeka kwa tope na pia hupelekea kukauka, mfano katika msimu wa Mwaka 1999/2000, 2009/2010 na 2014/2015 bwawa lilikauka. Hali hii inatokana na umri wa Bwawa ambao ni zaidi ya miaka 60, pamoja na upatikanaji wa mvua kwa mwaka husika. Kukauka kwa Bwawa huchangia kuleta uhaba wa maji katika Manispaa na pia huipunguzia Mamlaka ya maji kipato cha fedha kutoka kwa wateja wetu na hasa maeneo ya Ipuli, na Magereza.

### 1.2.2 Bwawa la Igombe

Chanzo ambacho ni tegemeo la Manispaa ya Tabora kwa sasa ni Bwawa la Igombe ambalo liko km 20 Kaskazini Magharibi mwa Manispaa ya Tabora. Bwawa hili lilikamilika ujenzi mwaka 1958, na kuanza kutumika mwaka 1960. Bwawa la Igombe lina uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo milioni 47 ambapo eneo linalokusanya maji (catchment area) ni kiasi cha km za mraba **4,200.**

### 1.2.3 Utunzaji wa Vyanzo vya Maji

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Tabora, inashirikiana na wadau mbalimbali wa Maji kama vile Serikali ya Mkoa, Wilaya, Halmashauri ya Manispaa, Wakala wa Misitu nchini, ofisi ya Bonde la Ziwa Tanganyika, vyombo vya Ulinzi na Usalama, Wananchi kwa ujumla na Serikali za Vijiji vinavyozunguka maeneo yenye rasilimali za Maji kuhakikisha ustawi wa vyanzo vya maji kwa kufanya yafuatayo:-

i. Kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka hifadhi ya bwawa, kuhusu njia mbadala za kupata kipato kupitia hifadhi yam situ na bwawa, bila kuleta mazara, kama vile ufugaji nyuki.
ii. Kuweka mipaka katika maeneo ya hifadhi za rasilimali za Maji.
iii. Kupanda miti katika maeneo yanayozunguka bwawa la Igombe.
iv. Kushiriki katika ukarabati wa majosho kwa ajili ya unyweshaji wa mifugo
v. Kuzuia uvunaji holela wa miti ndani ya hifadhi za mabwawa ya Maji.
vi. Kuzuia uvuvi wa kutumia sumu ndani ya mabwawa ya Maji.
vii. Kuhamasisha wananchi kuacha kutumia mbolea zenye chumvi chumvi hasa wale waishio jirani na bwawa la Maji.

viii. Kuzuia shughuli za kilimo ndani ya hifadhi ya mabwawa kwa ajili ya kupunguza wingi wa mchanga unaoingia bwawani wakati wa masika.
ix. Kuzuia shughuli za utafutaji wa madini katika maeneo ya bwawa la Igombe.
x. Kufanya doria za mara kwa mara kwenye eneo la hifadhi na kuchukua hatua za kisheria kwa wale wanaobainika kuvunja sheria.

Pamoja na jitihada hizi bado ipo changamoto kubwa ya uvamizi wa vyanzo ambapo kunashughuli za kibinadamu kama vile kilimo, uvuvi, malisho ya Mifugo, kukata miti na uchomaji moto majani katika hifadhi mambo ambayo ni hatari kwa mazingira ya hifadhi kwani yana haribu uoto wa asili wa hifadhi ya vyanzo.

## 1.3 HALI YA MIUNDO MBINU ILIYOPO.

### 1.3.1 MABOMBA YA MAJI SAFI

Mamlaka ya Maji inamiliki mabomba ya chuma na plastiki ya Majisafi yenye urefu wa **Km. 300** yaliyo na vipenyo kuanzia **mm 80** hadi **mm 600**. Sehemu ya mabomba hayo yamechakaa na vipenyo vyake vimepungua kutokana na kujaa kutu. Hali hii husababisha Mamlaka kushindwa kufikisha Maji katika baadhi ya maeneo mapya yanayoendelezwa na pia huchangia kusababisha upotevu wa Maji wakati mabomba hayo yanapopasuka.

### 1.3.2 MTANDAO WA MAJITAKA

Manispaa ya Tabora unao mtandao wa majitaka wenye urefu **kilomita 20** na malambo makubwa **matatu (3)** ya kupokea majitaka. Miundombinu hii inahudumia asilimia **6.2** ya wakazi waishio Manispaa ya Tabora.

### 1.3.3 MATENKI YA KUHIFADHI MAJI.

Mamlaka inayo matenki matatu ya kuhifadhia maji yenye uwezo wa kuhufadhi mita za ujazo **5,865** eneo la Kazehill**.** Matenki haya yaliyojengwa katika vipindi tofauti, tenki la kwanza lenye ujazo wa **mita 1,365** lilijengwa mwaka **1958,** tenki la pili lenye ujazo wa **mita 2,250** lilijengwa mwaka 1983 na tenki la tatu lenye ujazo wa **mita 2,250** lilijengwa mwaka 2001 kupitia Mradi wa USRP. Katika mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria

tunatarajia kujenga matenki matatu mapya yenye uwezo wa kihifadhi mita za **ujazo 17,000** ambayo itafanya jumla ya uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo **22,865**.

## 4.0 MAFANIKIO YA KIUTENDAJI YALIYOFIKIWA NA MAMLAKA HADI KUFIKIA JUNI 2017

Mamlaka tangu ianze kufanya kazi rasimi imeendelea kujitahidi kuboresha huduma ya Maji katika Mji wa Tabora na mafanikio yaliyo kwisha patikana hadi Machi 2016 ni kama ifuatavyo:

- Kuongezeka mtandao wa Majisafi takribani **km 30** katika maeneo ya Cheyo, Kwihara, Kidato, (hivyo kufanya jumla ya km **300** kwa sasa).
- Kungeza uwezo wa uzalishaji kufikia lita 30,000,000
- Kuongeza ubora wa maji kufikia kiwango cha WHO
- Kuongeza hali ya upatikanaji wa Maji na kufikia masaa 23
- Kuendelea kuwafungia wateja wote dira za maji
- Kutuma ankra na kulipia kwa njia ya mtandao
- Mapato ya Mamlaka yameongezeka na kufikia kutoka wastani wa Shilingi **milioni 20** kwa mwezi mwaka 1998 hadi kufikia shilingi **milioni 338** kwa mwezi.
- Makusanyo ya mapato yameongezeka kutoka wastani wa shilingi **milioni 12** kwa mwezi mwaka 1998 hadi kufikia wastani wa shilingi **milioni 320** kwa mwezi sawa na **asilimia 89** ya maduhuli ya mwezi.
- Mamlaka imeendelea kupata hati safi tangu kuanzishwa kwake
- Kufunga mita kubwa za Maji katika vituo vya uzalishaji na maeneo yaliyotengwa kikanda, ili kubaini kiasi cha Maji yanayozalishwa na kiwango cha upotevu wa Maji kwenye maeneo yaliyotengwa kikanda. Hadi sasa tunazo DMA 4 zinazofanya kazi kikamilifu.

## 5. CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO

Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa hapo juu, zipo changamoto mbalimbali zinazo ikabili Mamlaka kwa sasa katika kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira. Baadhi ya changamoto pamoja na mikakati ya kukabiliana zimeainishwa kwenye jedwali hapa chini:-

| S/N | CHANGAMOTO | MIKAKATI | Maoni/Mapendekezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya maji ambavyo kiasi kikubwa hutegemea hali ya mvua isiyo tabilika kutokana na mabadiliki ya hali ya hewa, ambapo kutokana na mvua kutokuwa nyingi kwa mwaka huu kupepelekea kupungua kwa kina cha maji kwenye mabwawa ya Kazima na Igombe na hivyo kuleta changamoto kwenye uzalishaji wa maji katika vituo hivi | Katika mpango wa muda mrefu Serikali inaendelea na mchakato wa kuleta maji ya Ziwa Victoria katika Mji wa Tabora, pia bado tunaendelea na kuangalia vyanzo mbadala kama vile maji chini ya ardhi. | Serikali kupitia Wizara ya maji kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi wa kuleta maji ya Ziwa Victoria katika Miji ya Tabora, Nzega, Igunga na hatimaye Mji wa Sikonge. |
| 2. | Uvamizi, Uchafuzi na uhabifu wa mazingira kwenye vyanzo vya maji kwa kuendelea kwa shughuli za kibinadamu. | Kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na ofisi ya Bonde la Ziwa Tanganyika, Serikali kuu, wakala wa misitu, Serikali za vijiji na Serikali kuu, pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama katika kutunza mazingira kwenye vyanzo | Wadau mbalimbali kushiriki katika suala la utunzaji wa mazingira kwani hili ni suala mtambuka. |
| 3. | Maeneo mapya ya Mji yanayoendelezwa kwa kasi kutokuwa na mtandao wa bomba ikilinganishwa na uwezo wa | Maeneo yote ya ndani ya Manispaa yatawekewa mtandao wa bomba kupitia | Wizara kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Mamlaka kifedha kulaza mabomba, hususani maeneo ya Mwinyi, Ipuli, Mtendeni, Cheyo, Kariakoo, Itetemia, Kipalapala ,na Malolo | mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria, ambapo mtandao mpya wa bomba wa zaidi ya km 250 utawekwa. Pia Mamlaka inafanya taratibu za kuchukua mkopo wa TZS 500,000,000 kutoka CRDB ili kulaza takribani **km 26** katika maeneo ya Usule, Kidato, Simbamwene kuongeza mtandao umbali wa km 21, katika maeneo ya Ipuli-Bonana, Kariakoo, Rwanzali na Skanda. | ili huduma ya maji kuwafikia wakazi wengi wa maeneo ya Manispaa. |
| 4. | Upotevu mkubwa wa maji unaofikia asilima **40** kwa sasa. | Kuendelea kuondoa bomba chakavu zilizobaki katika ukarabati wa awamu ya kwanza ya ukarabati, ambapo bado km 30. Kuendelea kuanzisha DMA kwa maeneo yaliyosalia na kuyasimamia kikamilifu, kwa kuweka matisha kwa kila eneo lililotengwa kikanda kulingana na ufanisi wake. | Wizara kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria, ampapo takribani km 30 za bommba chakavu zitabadilishwa. |
| 5. | Taasisi nyingi za Serikali kutolipa kwa wakati madeni. Hadi kufikia Marchi, 2017, Mamlaka ilikuwa inazidai taasisi za serikali **Tsh. 2,887,519,337.03 (JWTZ-** | Kuendelea kufuatilia kwa karibu kwa kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha kuwa Taasisi za Serikali zinalipia madeni yao kwa | Tunaiomba Wizara itusaidie kuwasiliana na Wizara ambazo Taasisi zake zimekuwa hazilipi matumizi ya maji kwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **2,476,756,369; Jeshi la Kujenga Taifa-2,438,020; Jeshi la Magereza-107,665,075; Jeshi la Polisi-300,659,873.03**) | wakati. | wakati kama vile JWTZ na polisi, ikibidi kuangalia uwezekano wa madeni haya kulipia moja kwa moja kutoka hazina, mara baada ya madeni haya kuthibitishwa na watumiaji na Wizara husika. |
| 6. | Kupanda kwa gharama za uzalishaji na uendeshaji kutokana na gharama za uzalishaji wa maji kulipiwa VAT kama vile umeme. | Mamlaka iko katika mchakato wa kuandaa mpango biashara ili kuweza kuangalia marekebisho ya bei ili ziendane na gharama halisi. | Tunaiomba Serikali kuangalia upya Sheria ya Kodi ya ongezeko la thamani hususani kwenye gharama za umeme na ilikumpunguzia mwananchi mzigo wa kulipia huduma hii muhimu. |
| 7. | Ufinyo wa mtandao wa Majitaka ambao unasababisha wakazi wengine kutonufaika na huduma hii. | Kuendelea kushirikiana na Sekta Binafsi pamoja na Manispaa ya Tabora kupokea taka zinazo-kusanywa na magari kutoka kwenye makazi ya watu na kumwagwa kwenye malambo ya kutibia taka za aina hii yaliyopo karibu na Tabotext.<br><br>Kuendelea kutafuta wafadhili kwa ajili ya kutekeleza kazi zilizoainishwa kwenye Mradi wa WSDP kwa ajili ya kuongeza mtandao wa majitaka katika maeneo mbalimbali ya mji | Serikali kupitia Wizara ya Maji kusaidia kupatikana upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa kuondoa Majitaka kaatika Manispaa ya Tabora na hasa ukizingatia ongezeko la majisafi litakaloongezeka baada ya Mradi wa kuongeza uzalishaji Igombe na Maji ya Ziwa Victoria. |

## 6.0 UBORESHAJI WA HALI YA HUDUMA YA MAJI MANISPAA YA TABORA

### 6.1 KAZI ZILIZOFANYIKA

Katika jitihada za kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Tabora ilitekeleza kazi mbalimbali katika mipango ya Muda mfupi ambazo zilikuwa zimeainishwa kwenye Mpango Biashara wa Mamlaka wa miaka 3 ulioishia Juni 2017, ambao ulihusisha miradi ya **SECO** na **WSDP**.

Serikali ya Uswisi, Kupitia Shirika lake la Maendeleo la SECO, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mamlaka ya maji Tabora, ilitekeleza kazi mbalimbali kuanzia mwaka 2008 hadi 2013 katika awamu zifuatazo:

Katika kipindi cha 2008 hadi 2011, kiasi cha **shilingi bilioni 1.6** kilitolewa na Serikali ya Uswisi ambazo zilitumika katika Ununuzi na ufungaji wa dira kubwa 26, upimaji wa sampuli za maji ya bwawa la Igombe kwa Mkemia mkuu Mwanza na nchini Uswisi, Ununuzi wa vifaa vya maabara na vitendea kazi kama vile computer kwa ajili yakituo cha Igombe na Ufungaji wa mfumo mpya wa utoaji ankra za wateja, uliounganishwa na mfumo wa uhasibu, ili kutoa ankra sahihi na kupunguza malalamiko kwa wateja.

Pia katika kipindi hicho, Mamlaka ilipokea kiasi cha **shilingi za kitanzani milioni 345.2** kutoka Wizara ya Maji, ikiwa ni mchango wa Serikali katika kutekeleza mradi wa SECO ambazo zilitumika kubadilisha mtandao wa bomba za zamani, katika barabara ya Hill na Kilimatinde kata ya Cheyo, **km 3.4** kwa ili kudhibiti upotevu wa maji pamoja na kununua na kufunga pampu mbili mpya katika kituo cha Igombe kusaidia kuongeza uzalishaji wa maji na kufikia **mita za ujazo 15,000** kwa siku.

Mnamo mwaka 2010 Serikali ya Uswisi, Kupitia Shirika lake la Maendeleo la SECO ilitoa **Dola za Marekani Million 4,841,790.89 sawa na shilling za kitanzania billion 7.5** ambazo zilitumika hadi 2013 katika kutekeleza kazi zifuatazo:

i) Kubadilisha bomba chakavu, katikati ya mji hususani maeneo ya Bachu, Gongoni, Kanyenye, Chemchemi, Kitete, umbali wa km 27

ii) Ununuzi na ufungaji wa dira za maji kwa wateja wetu wote (dira 5,000)

iii) Ununuzi na ufungaji wa pampu moja mpya ya kuchukua maji bwawani na kwenda kwenye machujio, yenye uwezo wa kusukuma maji mita za ujazo 700 kwa saa.
iv) Ununuzi na ufungaji wa pampu moja mpya ya kusukuma maji yaliyosafishwa kuja Mjini, yenye uwezo wa mita za ujazo 450 kwa saa.
v) Ukarabati wa kituo cha kuchukulia maji, ili kuzuia tope linaloingia sehemu hii.
vi) Kujenga mfumo wa kuweka dawa aina ya "chlorine" katika kituo cha Igombe na kujenga kituo cha kuongeza dawa ya kutibu maji maeneo ya TABOTEX ili kulinda ubora wa maji kwa watumiaji (Post Chlorination)
vii) Kununua na kufunga Transfomer mbili kwa ajili ya kituo cha Igombe
viii) Kuweka boma la mm 500, urefu wa km 2.7 kutoka Igombe kuelekea Mjini Tabora
ix) Ukarabati wa chujio tatu zilizopo Igombe ili baadaye zitumike kama matanki ya kihifadhi maji yaliyosafishwa.

Sambamba na mradi wa SECO hapo juu, kupitia program ya kuendeleza sekta ya maji nchini Water sector Development Programu (WSDP), Mamlaka ilianza kutekeleza kazi za mradi wa kukarabati na kupanua machujuo ya maji katika kituo cha Igombe kuanzia mwaka 2013, ili kuongeza uwezo wa uzalishaji kutoka mita za uajazo **15,000** wakati huo na kufikia mita za **ujazo 30,000 kwa siku**, ambapo kazi mbalimbali zimetekelezwa kama zilivyo orodheshwa hapa chini.

i) Kufunga pampu mbili zenye uwezo wa kusukuma mita za ujazo 350 kwa saa kila moja kituo cha kuchota maji ghafi (Low lift station)
ii) Kufunga transfoma ndogo ya 200kVA eneo ka kuchukulia maji ghafi
iii) Ujenzi wa bomba la mm 400 urefu wa Mita 288
iv) Kukarabati chujio la maji la zamani lenye uwezo wa mita za ujazo 15,000 kwa siku.
v) Ujenzi wa chujio jipya lenye uwezo wa mita za ujazo 15,000 kwa siku.
vi) Kufunika matanki matatu ya maji yaliyobadilisha kutoka kuwa machujio na kuwa matenki ya kuhifadhia maji katika mradi wa SECO
vii) Kufunga pampu moja kituo cha kusukuma maji kuelekea mjini Tabora (High lift station) na

viii) Kufunga Transformer moja kubwa ya 800kVA

Utekelezaji wa kazi hizi umekamilika kwa **thamani ya Dola za Marekani 4,737,837.76 (sawa na Shillingi za kitanzania Billioni 7.5)** mnamo Marchi, 2016 na kuwa na muda wa matazamio hadi Marchi, 2017 ambapo umeongezwa kwa baadhi ya kazi hadi June 2017.

## 6.2 MATOKEO BAADA YA KAZI KUKAMILIKA

Baada ya kukamilika miradi yote miwili yaani SECO na WSDP katika kuboresha huduma ya maji Manispaa ya Tabora imeleta mafanikio yafuatayo:-

1. Kuongezekeka kwa uwezo wa kuzalisha maji kutoka mita za ujazo **15,000,** 2013 na kufikia **mita za ujazo 30,0000 kwa siku** ambayo inazidi mahitaji hadi kufikia **mwaka 2020.**
2. Wastani wa wateja kupata maji kwa siku utaongezeka kutoka wastani wa **masaa 12** na kufikia **masaa 19** na hivyo kuondoa hali ya mgao.
3. Ubora wa maji yanayozalishwa kuongezeka
4. Kufungia wateja wetu wote dira za maji na hivyo kupunguza malalamiko ya kupelekewa Ankara zisizo sahihi.
5. Kuongeza kivutio na uhakika wa maji kwa wawekezaji katika mji wetu wa Tabora.
6. Kuiongezea Mamlaka mapato yatokanayo na mauzo ya huduma zetu na kuweza kujiendesha, bila kutegemea ruzuku ya Serikali
7. Wananchi kushiriki zaidi kwa shughuli za kiuchumi na kijamii, kuliko kutumia muda mwingi kutafuta maji

## 7. HITIMISHO

Kama nilivyoeleza hapo juu kuhusu mafanikio katika miradi hii miwili mikubwa ya maji, lakini bado ipo changamoto ya kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya maji (maji juu ya ardhi- mabwawa), ambavyo kwa kiasi kikubwa hutegemea hali ya mvua ambayo haitabiliki kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, mathalani kwa kuwa msimu wa mvua uliopita haukua na mvua ya kutosha na hivyo kupelekea kina cha maji kupungua saana katika mabwawa yote mawili ambayo ina athiri hali ya ubora wa maji katika vituo

vya uzalishaji. Kwa kuona hali hii inapelekea kuwa na uhitaji wa vyanzo vingine vya uhakika kama vile maji kutoa Ziwa Victoria ili kuwa na uhakika wa huduma ya maji katika Mji wa Tabora na pia kuongeza huduma ya uondoaji wa majitaka ili kudhibiti uchafunzi wa mazingira kutokana na ongezekeko la maji safi katika Manispaa ya Tabora.

Pia kutokana na uvamizi wa vyanzo na shughuli za kibinadamu zinazoendelea na hivyo kupelekea uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji kwa hiyo tunatoa wito wa wadau mbalimbali ikiwemo kamati ya ulinzi ya Wilaya tushirikiane kwa pamoja kuchukua hatua sitahiki za haraka kunusuru hali hii ambayo inawezaa kupelekea ukame wa vyanzo.

**Maji ni Uhai na usafi wa mazingira ni utu, kwa pamoja tushirikiane kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira Tabora**